

PIARC

+Nchi 120

+Wataalamu 1,200

+Kamati za ufundi 20

Tangu mwaka 1909

# USHIRIKIANO WA KIMATAIFA WA BARABARA NA UCHUKUZI KWA NJIA YA BARABARA

# MADA ZETU

## MADA ZOTE ZINAZOHUSIANA NA BARABARA NA UCHUKUZI KWA NJIA YA BARABARA

- USALAMA BARABARANI
- MATUMIZI MAPYA YA BARABARA
- SERA YA UCHUKUZI
- UGHARAMIAJI
- USALAMA
- UTENDAJI WA MAMLAKA ZA UCHUKUZI
- NJIA ZA WATEMBEA KWA MIGUU.
- UENDESHAJI WA NJIA YA BARABARA YA CHINI KWA CHINI
- MAZINGIRA
- MAGARI YANAYOTUMIA MIFUMO YA KIMTANDAO YA INTANETI
- MIKAKATI YA MATENGENEZO NA UENDESHAJI
- SHUGHULI ZA MTANDAO
- UCHUKUZI WA MIZIGO
- UDHIBITI NA USIMAMIZI WA MAAFA
- HUDUMA MAJIRA YA BARIDI
- KUKABILIANA NA CHANGAMOTO
- MADARAJA
- UCHUKUZI KWA KUTUMIA TEKNOLOJIA YA MAWASILIANO
- BARABARA ZA VIJIJINI
- KAZI ZA UJENZI
- MWINGILIANO WA NJIA ZA UCHUKUZI
- USIMAMIZI WA RASILIMALI ZA BARABARA
- KUSAFIRI MAENEO YA MIJINI
- ...







**Barabara** ni njia ya zamani zaidi ya usafiri na hadi sasa matumizi yake ni zaidi ya asilimia 80 ya matumizi yote ya njia zote za usafiri katika nchi nyingi. Hata hivyo, njia ya usafiri ya Barabara inakabiliwa na ongezeko la changamoto mbalimbali ikiwa ni pamoja na mahitaji ya usafiri, maendeleo mapya, mashinikizo ya kijamii, na upungufu wa fedha kukidhi mahitaji.

Duniani kote wataalamu, watafiti na watendaji wanashugulikia masuala ya uchukuzi kwa njia ya barabara kwa ajili ya kuandaa na kutekeleza mbinu muafaka zaidi.

Katika mchakato huu, **Ushirikiano wa Kimataifa** ni nyenzo muhimu.

- **Badala ya kuanzisha tena mbinu inayoonekana kuwa bora, mbinu iliyopo hujadiliwa kwa pamoja katika mikutano na kushirikisha wadau, ambapo huokoa muda na fedha,**
- **Pia, mawazo yanaweza kuchambuliwa , jambo ambalo huwezesha upatikanaji wa dhana mpya,**
- **Ushirikiano huu pia huwawezesha washiriki kuhamasisha utaratibu unaotumika kwenye nchi zao.**

**Chama cha Barabara Duniani (PIARC)**, kilianzishwa mwaka 1909 kwa ajili kuwezesha aina hii ya ushirikiano kwenye masuala yote yanayohusiana na barabara. Chama hiki **hakijihusishi na masuala ya kisiasa na hakizalishi faida**. Kinaunda mtandao wa wataalamu wa barabara duniani ambapo huwapatia wataalamu hao mbinu za kufanya kazi kwa ushirikiano, na kuchapisha mapendekezo na ripoti zao. Mambo haya yote hufanyika katika muktadha wa umoja na uchukuzi endelevu.

Huduma na bidhaa zetu zinapatikana kwa urahisi na zinazingatia matarajio na matamkwa ya wanachama wetu, ambao kimsingi ni pamoja na serikali za nchi zaidi ya 120.

# DHAMIRA YETU

## KUANZISHA JUKWAA LA KIMATAIFA LA KUCHAMBUA NA KUJADILI MASUALA YANAYOHUSIANA NA BARABARA NA UCHUKUZI KWA NJIA YA BARABARA

- Mkutano Mkuu wa Shirikisho, ambao umekuwa ukifanyika kila baada ya miaka minne tangu mwaka 1908,
  - mwaka 2019 Abu Dhabi (Jumuiya ya Nchi za Falme za Kiarabu),
  - mwaka 2023 Prague, katika Jamhuri ya Czech.

XXVII[TH] WORLD ROAD CONGRESS PRAGUE 2023


- Mkutano Maalum wa Kimataifa wa Masuala ya Barabara wa Majira ya Baridi
  - mwaka 2018 Gdansk nchini Poland;
  - na mwaka 2022 Calgary nchini Canada

CALGARY 2022 CANADA

- Wataalamu wa kimataifa 1,200
- Vikao vya Kamati za Kitaalamu na Vikosi kazi zaidi ya 20
- Mikutano ya kisheria ya Kamati na Baraza Tendaji
- Mikutano ya ngazi ya Kitaifa (Kamati za Kitaifa)

## KUBADILISHA UZOEFU WA UTENDAJI BORA NA KUASISI MFUMO BORA WA UPATIKANAJI WA TAARIFA ZA KIMATAIFA

- Uchapishaji wa ripoti mbalimbali, zinazopatikana bure- 1 kila mwezi




- Jarida la «*Routes/Roads*» la lugha tatu linalochapishwa kila robo mwaka
- Mikutano : Njia za barabara za chini kwa chini, Sifa la tabaka la juu la barabara



- Mihtasari (Miradi Maalum)

## KUCHUKUA HATUA ZA UPENDELEO KWA NCHI ZINAZOENDELEA NA ZILIZOPO KATIKA KIPINDI CHA MPITO

- Mahitaji yanajumuishwa katika mada tunazotumia
- Semina za kimataifa – semina moja kwa wika sita
- Vikosi kazi vya kikanda
- Taratibu za misaada ya kifedha



## KUANDAA NA KUKUZA MBINU BORA ZINAZOWEZESHA KUFANYA MAAMUZI KUHUSIANA NA BARABARA NA UCHUKUZI KWA NJIA YA BARABARA

- Kamusi yetu ya barabara ya lugha mbalimbali ya mtandaoni
- HDM-4: Mfumo wa kompyuta unaohusu sera ya matengenezo ya barabara na uchambuzi wa uwekezaji
- DG-QRAM: Nyenzo inayoshughulikia uchukuzi wa bidhaa hatarishi kwenye njia za barabara za chini kwa chini
- Miongozo maalum inayopatikana mtandaoni: usalama barabarani,shughuli za njia ya barabra ya chini kwa chini , usimamizi wa rasilimali za barabara, uendeshaji wa shughuli za barabara/ Uchukuzi kwa kutumia teknolojia ya mawasiliano ya kimtandao

# TUNAFANYAJE KAZI ?




**Kamati za Ufundi** na **Vikosi Kazi** ndizo sehemu za PIARC zinazoonekana zaidi.

Hukutanisha zaidi ya wataalamu 1,200 kutoka duniani kote, na hivyo kuifanya PIARC **kuwa mtandao mkubwa zaidi duniani wa watalaamu wa barabara**. Majukukmu yao yanajikita zaidi katika uendeshaji wa mikutano miwili ya mwaka na semina mbalimbali katika nchi zenye uchumi wa chini na uchumi wa kati, zinazohitimisha uchapishaji ripoti za mada za kitaalamu zinazopewa kipaumbele.

Sehemu kubwa ya bidhaa zetu zimeandikwa kwa lugha ya Kiingereza, Kifaransa, na Kihispania – ambazo ndio lugha tatu za kazi za PIARC - na wakati mwingine lugha nyingine pia hutumika.

# UBIA

**PIARC** inapendelea sana kuwa na ubia kwa matarajio ya kujenga barabara mahali ambapo barabara hizo zinakuwa sehemu muhimu ya mfumo wa uchukuzi , unaohakikisha kwamba bidhaa zetu zinasambazwa kwa kiwango kikubwa, unaochangia katika kubadilishana uzoefu wa utendaji bora, unaotuwezesha kuzifikia kwa urahisi jamii zinazohitaji barabara, unaoratibu mipango ya utekelezaji na kubuni miradi ya pamoja.

**Kamati za Kitaifa za PIARC:** vyama vya barabara vya kitaifa, vilivyoanzishwa kwenye ngazi ya kitaifa katika nchi zaidi ya 40.

**Vyama vya barabara vya kikanda**: CEDR katika Bara la Ulaya, AGEPAR katika nchi zinazozungumza Kifaransa katika Bara la Afrika, REAAA katika Bara la Asia, na DIRCAIBEA katika Bara la Amerika ya Kusini.

**Mashirika ya maendeleo** ni pamoja na Benki ya Dunia, Benki ya Maendeleo ya Bara la Asia, Benki ya Maendeleo ya Amerika ya Kusini, n.k.

**Mashirika ya Kiufundi ya Kimataifa**: TRB (USA), Chama cha Utengenezaji wa Barabara za chini kwa chini (ITA – AITES), FISITA, n.k.

# KWANINI UJIUNGE NA PIARC ?

| SHIRIKI KATIKA | UPATIKANAJI WA TAARIFA ZETU |
|---|---|
| Matukio yetu | Jarida letu la «*Routes/Roads*» |
| Ushirikiano katika mada zinazohusiana na barabara ngazi ya kimataifa. | Maktaba yetu ya mtandaoni |
| Kamati za Ufundi na VikosiKazi | Kamusi yetu ya barabara ya mtandaoni |
| Kubaini masuala yanayohusiana na barabara. | Bidhaa zetu za Programu za kompyuta |

**Tunatoa aina kadhaa za uanachama: serikali za kitaifa; mamlaka za kikanda; makampuni au vyuo vikuu; wanachama binafsi.**

# TIMU YA PIARC

| Baraza | Rais | Kamati Tendaji | Sekretarieti Kuu ya PIARC |
|---|---|---|---|
| **Huwajibika Kusimamia Chama** | **Huchaguliwa na Baraza** | **Husimamia Chama** | **Huratibu shughuli zote** |
| Inaundwa na wajumbe kutoka kila nchi wanachama, wakiongozwa na Mjumbe Mkuu | Kwa kipindi cha miaka mine | Wakisaidiwa na Tume kadhaa | Makao Makuu Paris, nchini Ufaransa<br><br>Viongozi na wataalamu waliopatikana kutoka kwa baadhi ya nchi wanachama<br><br>Wafanyakazi |

# www.piarc.org

- Pakua machapisho yetu

- Tufuatilie kwenye mitandao ya kijamii

- Jisajili kwenye jarida letu

PIARC